



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb: Na. CHAL/L. D/4088

23.12.2025

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
TISEZA,  
S. L.P. 938,  
DAE ES SALAAM.**

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NAMBA 1 KITALU 18A MINDUKENE  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE.**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Awali eneo hili la Ardhi lilikuwa linamilikiwa kienyeji kama shamba na wananchi wazawa wapatao 11 ambao waliuza mashamba yao kwenye Kampuni ya **HONGDA TERRA ENERGY COMPANY LIMITED** ya S.L.P 20950 Dar es Salaam yenye ukubwa wa ekari 406.65. Wananchi hao ni kama ifuatavyo; Ndugu Msafiri Said Maduga ekari 10.13, Anna Paulo Mgugulo ekari 24.24, Said Ally Maduga ekari 2.32, Said Gweno Kuchigudi ekari 89.17, Jumanne Idd Mselemu ekari 227.39, Pascal Joseph Ernest ekari 29.72, Joseph Mhonde Mpiga ekari 10.23, Juma Elimu Kazi ekari 27.06, Mwajuma Said Mduga ekari 3.50, Shukuru Said Mduga ekari 5.74 na Said Fredrick Pendo ekari 7.24.

3. Kampuni hiyo ililipa stahili za mwananchi huyo kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji cha Mindukene.

4. Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji cha Mindukene tarehe **26.10.2025** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Tonga uliofanyika tarehe **26.10.2025** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **ekari 406.65**. Aidha, kwa kuwa ukomo wa Kijiji kugawa Ardhi ni ekari 50 tu, Kikao cha Kamati ya Kugawa Ardhi Wilaya kitafanyika mapema mwezi 1 mwaka 2026 baada ya kuundwa kamati mpya, (Muhtasari wa Halmashauri ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa kijiji na mikataba ya mauziano imeambatanishwa kwa marejeo yako).

5. Baadaye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Chalinze ilipokea barua ya tarehe 16/11/2025 ya kuomba kupimiwa ardhi hiyo. Wataalam walitembelea eneo hilo na kubaini halina mgogoro wowote na baadaye ulibuniwa mchoro wa Mipango Miji Nambari **TP. DRG. NO.PWA/02/475/2025** ulioidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipangomiji na Vijiji Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa matumizi ya **Kiwanda (Use Group "N" Industry Use classes (a) and (b) as defined in UPA No. 8 of 2007.**"


6. Aidha upimaji wa ardhi hiyo ulifanyika na ramani kupata kibali cha Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyosajiliwa kwa namba **PWNSP00001482** na kupatikana kiwanja namba **1 kitalu "18A" MINDUKENE**.

7. Kwa kuwa kampuni inayoomba ardhi ni ya kigeni; Kampuni ya **"HONGDA TERRA ENERGY COMPANY LIMITED** ya S.L.P 20950 Dar es Salaam" imewasilisha:

- a. Mikataba ya mauziano ya Wananchi wazawa wapatao 11,
- b. Muhtasari wa Halmashauri ya Kijiji na Mkutano mkuu wa Kijiji
- c. Udhibitisho wa uraia /pasi za kusafiria za Wakurugenzi,
- d. Certificate of incorporation of a Company,
- e. Certificate of registration,
- f. TIN number,
- g. Business License,
- h. Tax clearance certificate
- i. Ramani ya upimaji wa kiwanja Na 1 kitalu 18A

8. Kwa barua hii, nathibitisha kuwa kiwanja Namba 1 Kitalu 18A Mindukene hakina mgogoro wowote nawasilisha kwako kwa hatua zaidi. Utaratibu wa umilikishaji wa kiwanja hiki unasubiri kikao cha Kamati ya kugawa Ardhi ya Wilaya.

9. Natanguliza shukrani.

  
ARCHANUS A. KILAJA  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
CHALINZE.



Nakala kwa:

**HONGDA TERRA ENERGY COMPANY LIMITED,** kwa ufuatiliaji  
S.L. P. 20950,  
**DAR ES SALAAM.**

Afisa Mtendaji wa Kijiji,  
Kijiji Cha Mindukene.

kwa taarifa